

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu: +46 8 732 24 30/31  
Fax: +46 8 732 24 32  
Email: [mailbox@tanemb.se](mailto:mailbox@tanemb.se)  
Web: [www.se.tzembassy.go.tz](http://www.se.tzembassy.go.tz)

Ubalozi wa Tanzania  
Näsby Allé 6  
183 55 Täby  
Stockholm  
Sweden  
12 Julai, 2023

**Kumb. Na: 38/605/01**

**Viongozi Wote,**  
Jumuiya za Watanzania (Diaspora)  
Waishio Nchi za Uwakilishi.

## **YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA NALA Inc. KWA WATANZANIA WOTE WAISHIO NJE (DIASPORA)**

Tafadhali rejeeni somo tajwa hapo juu.

2. Ubalozi umepokea barua kutoka Kampuni tajwa hapo juu ikiomba kutambulishwa kwa Watanzania na Jumuiya zote za Watanzania waishio katika nchi za Uwakilishi. Kampuni ya NALA Inc. inamilikiwa na Diaspora Mtanzania anayeitwa Bw. Benjamin Fernandes. Kampuni hiyo inatoa huduma za kutuma na kupokea fedha kupitia Benki na Mitandao ya Simu za Mkononi nchini Tanzania. Aidha, Kampuni hiyo hutoa huduma ya kutuma fedha katika nchi Ishirini na Moja (21) Ulimwenguni. Nchi hizo ni Austria, Cyprus, Estonia, Finland, Hispania, Ireland, Italia, Latvia, Lithuania, Luxembourg, Malta, Marekani, Slovakia, Slovenia, Ubelgiji, Ufaransa, Ugiriki, Uingereza, Uholanzi na Ureno.
3. Kwa nchi za Afrika, Kampuni ya NALA Inc. hutoa huduma ya kutuma na kupokea fedha nchini Tanzania, Rwanda, Kenya, Uganda, Senegal, Ghana na Nigeria. Hivyo, Ubalozi unapenda kuwajulisha Viongozi wote kuhusu Kampuni hii ili muweze kufikisha taarifa za huduma za kampuni hiyo kwa Diaspora wote waliopo katika maeneo yenu.
4. Ubalozi unatoa shukrani kwa ushirikiano wenu.

Grace A. Olotu  
**BALOZI**